# TAARIFA YA JAJI MKUU WA TANZANIA MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA KWENYE MKUTANO NA WAANDISHI WA HABARI KATIKA UKUMBI WA KITUO JUMUISHI–TEMEKE TAREHE 14 JANUARI, 2025 KUHUSU MAADHIMISHO YA WIKI NA SIKU YA SHERIA NCHINI MWAKA 2025

**MHE. DKT. MUSTAPHER SIYANI, JAJI KIONGOZI, MAHAKAMA KUU YA TANZANIA,**

**MHE. MWANABARAKA MNYUKWA, JAJI MFAWIDHI KITUO JUMUISHI–TEMEKE,**

**PROF. ELISANTE OLE GABRIEL, MTENDAJI MKUU, MAHAKAMA YA TANZANIA,**

**MHE. EVA KIAKI NKYA, MSAJILI MKUU, MAHAKAMA YA TANZANIA,**

**MHE. GEORGE HILLARY HERBERT, MSAJILI WA MAHAKAMA YA RUFANI,**

**MHE. CHIGANGA TENGWA, MSAJILI WA MAHAKAMA KUU,**

**BW. LEONARD MAGACHA, MTENDAJI MAHAKAMA KUU–KANDA,**

**BI. MARY SHIRIMA, MTENDAJI MAHAKAMA KUU–DIVISHENI,**

**NAIBU WASAJILI, WATENDAJI NA WATUMISHI WA KADA MBALIMBALI MLIOPO,**

**NDUGU WAANDISHI WA HABARI KUTOKA VYOMBO MBALIMBALI VYA NDANI NA NJE YA NCHI,**

**MABIBI NA MABWANA.**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

***Mahakama ya Tanzania!***

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kufika mahali hapa tukiwa na afya njema.

Pili, naomba nichukue fursa hii kuwatakia nyote HERI YA MWAKA MPYA 2025. Huu mwaka (2025) ni wa mwisho katika robo ya kwanza ya Karne ya Ishirini na Moja (21).

Tatu, nawashukuru Wahariri na waandishi wa Habari ambao mmefika mahali hapa kwani kila mara tunapokuwa na tukio kama hili mmekuwa mkiitikia wito wetu. Mahakama ya Tanzania inatambua kwa dhati kabisa kwamba nyie ni wadau muhimu sana katika kufikisha habari kuhusu kazi za Mahakama kwa umma.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Mahakama ya Tanzania ina jukumu la kikatiba la kutoa haki kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali. Katika kutimiza jukumu hilo la msingi, Mahakama ya Tanzania inaongozwa na Dira inayoelekeza **Utoaji Haki kwa Wakati na kwa Watu Wote** (*Timely and Accessible Justice for All*).

Katika kutekeleza Dira yake, Mahakama ya Tanzania imekuwa ikifanya maboresho kwenye huduma zake ili kutoa huduma bora inayomlenga mwananchi kupitia Mipango Mikakati na Programu za Maboresho.

Kwa sasa Mahakama ya Tanzania inatekeleza Mpango Mkakati wa PILI wa Miaka Mitano (2020/21–2024/25). Nguzo ya Tatu ya Mpango Mkakati unaoendelea kutekelezwa unalenga kuimarisha imani ya wananchi na ushirikishwaji wa wadau katika shughuli za Mahakama. Wahariri na waandishi wa Habari nyie ni kiungo muhimu cha kuhabarisha wananchi kazi za mahakama na kwa njia hiyo mnasaidia kujenga imani ya wananchi kwa Mahakama.

Katika kutekeleza Nguzo ya Tatu ya Mpango Mkakati, kila mwaka Mahakama huadhimisha WIKI YA SHERIA na SIKU YA SHERIA. SIKU YA SHERIA huashiria mwanzo wa shughuli za Mahakama kwa mwaka husika baada ya kumalizika kwa likizo ya Mahakama inayoanza kila tarehe 15 Desemba na kumalizika tarehe 31 Januari ya mwaka unaofuatia.

Kila Mwaka, Mahakama ya Tanzania hutenga WIKI na Siku Maalum na kuziita WIKI NA SIKU YA SHERIA kama wakati mahsusi wananchi kujifunza shughuli za Mahakama na zile za Wadau wa Mahakama.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Kama ilivyo kawaida kila mwaka wakati wa WIKI YA SHERIA, Mwaka huu 2025, zoezi la utaoji elimu litahusisha Wahe. Majaji, Wasajili, Naibu Wasajili, Watendaji na Mahakimu. Aidha, tutashirikiana na wadau wetu muhimu kama vile Tume ya Utumishi wa Mahakama, Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Tume ya Kurekebisha Sheria, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS).

Taasisi nyingine zitakazoshiriki katika kutoa elimu ni Ofisi ya Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Chama cha Majaji Wanawake (TAWJA), Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA), Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na wadau wengine.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Kwa kuzingatia kwamba maadhimisho ya Wiki ya Sheria yanafanyika siku za kazi ambapo wananchi wengi wanakuwa kwenye shughuli za utafutaji wa kipato, utoaji elimu mwaka 2025 umelenga kuwafuata wananchi karibu zaidi na maeneo yao wanayofanyia kazi tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Tutatoa elimu ya masuala mbalimbali ya kisheria kwenye maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi kwa kutumia magari maalumu yatakayokuwa yanahama kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Tutaongeza wigo wa utoaji elimu kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo ili kuwafikia wananfunzi wengi zaidi.

Ili kuhakikisha elimu inawafikia watu wengi zaidi tutaongeza wigo wa vipindi vya utoaji elimu kwenye vyombo vya habari kupitia luninga, redio na mitandao ya kijamii. Ni matumaini yetu kwamba utaratibu wa mwaka huu utatuwezesha kuwafikia wananchi wengi zaidi ambao wanahitaji kupata uelewa wa masuala mabalimbali ya kisheria.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Maadhimisho ya Wiki na Siku ya Sheria mwaka 2025 yatafanyika katika ngazi ya Kitaifa, Kanda za Mahakama Kuu, Divisheni za Mahakama Kuu, Mikoa na Wilaya zote nchini ambapo elimu ya masuala mbalimbali ya kisheria itatolewa katika maeneo mbalimbali.

Maadhimisho ya Wiki ya Sheria ni jukwaa maalum linaloikutanisha Mahakama na wadau wake muhimu hususani wananchi ili kutoa elimu ya shughuli zinazotolewa na Mahakama na wadau wake walio katika mnyororo wa utoaji haki.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Maadhimisho ya Wiki ya Sheria mwaka 2025 yataanza tarehe 25 Januari hadi tarehe 01 Februari, 2025 na SIKU YA SHERIA (LAW DAY) itakuwa ni tarehe 03 Februari, 2025.

Kitaifa, Mgeni Rasmi wakati wa uzinduzi wa WIKI YA SHERIA (LAW WEEK) tarehe 25 Januari 2025 anatarijiwa kuwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwenye Viwanja vya Mwalimu Nyerere (Nyerere Square) Jijini Dodoma.

Uzinduzi wa WIKI YA SHERIA utatanguliwa na Mbio Maalumu (*Fun Run*) za kilomita 10 ambazo zitaambatana na matembezi ya umbali wa kilomita tano kwa wale ambao watapendelea kutembea. Katika hizo mbio maalum na matembezi ya tarehe 25 Januari 2025, tutaongozwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Hafla ya Siku ya Sheria (LAW DAY) itafanyika kwenye Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma ambapo Mgeni Rasmi kwenye kilele cha Siku ya Sheria Nchini anatarajiwa kuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KAULI MBIU YA WIKI YA SHERIA NA SIKU YA SHERIA**

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Maadhimisho ya Wiki na Siku ya Sheria nchini yamekuwa yakiongozwa na Kaulimbiu kwa kuchagua eneo mahususi kwa lengo la kupata mjadala mpana katika eneo husika.

Ndugu zangu Wahariri na waandishi wa Habari, kama nilivyogusia awali, Mwaka huu 2025, ndio mwaka wa mwisho wa DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2025, na sasa hivi, Tanzania inajadili Rasimu ya DIRA YA Taifa ya maendeleo 2050.

Kwa hiyo, *KAULI MBIU YA WIKI NA SIKU YA SHERIA MWAKA HUU (2025)—itahusu DIRA 2050— "**Tanzania 2050: Nafasi ya Taasisi Zinazosimamia Haki Madai katika Kufikia Malengo Makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo**".*

Kwa takriban kuanzia Mwaka 2016, Mahakama ya Tanzania imekuwa ikifanya maboresho katika utoaji haki kupitia Mipango Mkakati na Programu za Maboresho ambazo ziliandaliwa kwa kuzingatia nafasi ya Mahakama ya Tanzania kama Taasisi tekelezi ya DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2025 itakayofikia ukingoni tarehe 31/12/2025.

Aidha, maboresho ya Mahakama yalilenga kuongeza ufanisi, weledi na uwazi katika utekelezaji wa jukumu la kikatiba la kutoa haki ikiongozwa na Dira ya Mahakama ya *Utoaji Haki kwa Wakati na kwa Watu Wote'* kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazosimamia Haki Madai.

Katika kufanya hivyo, Mahakama ya Tanzania inaweza kujipambanua kuwa ni mmoja wa watekelezaji wakubwa wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 ambayo itafikia ukomo tarehe 31/12/2025.

*Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050*

Hapana shaka yoyote kuwa, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni dira kuu ya kitaifa itakayoonyesha njia ya Kila Taasisi kufuata na kuzingatia ili kufikia ndoto kuu ya Tanzania kuwa **taifa lenye maendeleo yanayolingana na NCHI YENYE UCHUMI WA KIPATO CHA KATI NGAZI YA JUU au zaidi.** Katika wiki na siku ya Sheria, Taasisi zinazosimamia HAKI-MADAI tutakumbushana kuwa hatuwezi kukwepa wajibu wetu wa kufanya MAGEUZI MAKUBWA ya kitaasisi (ikizingatiwa ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaokadiriwa na Rasimu ya Dira 2050 kufikia milioni 140.

Kauli Mbniu inatukumbusha Mahakama na taasisi zote zinazosimamia HAKI-MADAI, kuwa Dira ya Maendeleo 2050 limeainisha mipango, mikakati tunayotakiwa kuitafakari, kuifahamu na kuitekeleza, kwa kuzingatia rasilimali zitakazotumika ili kufikia malengo **taifa lenye maendeleo yanayolingana na NCHI YENYE UCHUMI WA KIPATO CHA KATI NGAZI YA JUU au zaidi**.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Wiki ya Sheria ni Wakati mzuri kwa Taasisi katika Haki Madai kujadili namna ya kuiga mabadiliko makubwa yaliyofanywa katika Taasisi za nchi nyingine zilizofanikiwa kufikia **NCHI ZENYE UCHUMI WA KIPATO CHA KATI NGAZI YA JUU.** Muda wa kujadiliana kabla ya kufanya hayo mabadiliko makubwa ya kitaasisi na utoaji wa huduma, ni mfupi kabla ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kuanza kutumika Tanzania kuanzia tarehe 01 Januari 2026.

Hivyo basi, Kaulimbiu ya WIKI na SIKU ya Sheria kwa mwaka huu (2025) inalenga:

- Kuzitahadhari Taasisi zinazosimamia Haki-Madai kuhusu umuhimu wa kufanya matayarisho ya hayo mabadiliko

makubwa ili yaweze kuwa wezeshi na ziepuke kuwa vikwazo kwa Tanzania kuwa Taifa lenye maendeleo yanayolingana na nchi zenye Uchumi wa KIPATO CHA KATI NGAZI YA JUU au zaidi kulingana na matarajio ya Dira 2050.

- Kuzihamasisha taasisi katika Haki Madai kutafuta wataalamu wa MABADILIKO NA MABORESHO makubwa ya Kitaasisi ili ziwasaidie kubadili BUSINESS PROCESS zao kutoka BUSINESS AS USUAL hadi BUSINESS PROCESS REENGINEERING.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Kwa kuangalia orodha ya wadau tuliowaalika, wananchi watapata fursa muhimu katika Wiki ya Sheria kupata elimu mbalimbali kuhusu huduma na taratibu za utoaji huduma, na pia, kupata msaada wa Kisheria, Uandishi wa Wosia, Usimamizi wa Mirathi na huduma nyingine.

Wananchi watapata fursa ya kuzungumza, kuuliza maswali na kujadiliana na Maafisa wa Mahakama kwa lengo la kujifunza huduma mbalimbali katika utoaji haki ikiwa ni jukumu la msingi la Mahakama.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Napenda kutoa rai kwa wananchi na wadau wote wa Sheria kutembelea sehemu zote zitakazoandaliwa kwa ajili maadhimisho ya Wiki ya utoaji elimu ya sheria nchini kote.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Mkiwa wadau wetu muhimu katika utekelezaji wa masuala mbalimbali, ninawaomba mtusaidie kufikisha ujumbe wa MABADILIKO MAKUBWA yanayotarajiwa kutoka katika kila Taasisi zinazosimamia HAKI-MADAI ili hizi Taasisi ziwezeshe wananchi wa Tanzania kuyafaidi maendeleo yanayolingana na Tanzania kama mojawapo wa nchi zenye Uchumi wa KIPATO CHA KATI NGAZI YA JUU au zaidi kulingana na matarajio ya Dira 2050.

Fikisheni ujumbe huu kwa umma ili wananchi wafike katika maeneo mbalimbali nchini ambako utoaji elimu utafanyika pamoja na kushiriki katika siku ya kilele ambapo katika ngazi ya kitaifa, Mheshimiwa Rais anatarajiwa kushiriki.

***ASANTENI KWA KUNISIKILIZA***